

HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Mkoa wa Singida:
Simu No. 0262502252/2237
Fax No. 0262502316
E-mail: ded.singidadc@singida.go.tz



S.L.P. 27,
SINGIDA.

18, Mei, 2021

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA CLERK OF WORK.

Halmashauri ya Wilaya ya Singida inatarajia kujenga jengo la Ofisi ya Halmashauri lenye Ghorofa moja katika eneo la Kijiji cha Mwachango. Kwa kuzingatia Muongozo wa ujenzi imeelekezwa kuwa Halmashauri inapaswa kuajiri msimamizi wa kazi. Hivyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa na wenye nia kutuma maombi ya nafasi ya kazi ya **Msimamizi wa Kazi (Clerk of Work)** kwa kuzingatia vigezo na maelekezo yaliyopo katika tangazo hili.

1. MSIMAMIZI WA KAZI (CLERK OF WORK):

a) Sifa:

- Awe professional Engineer, Architect au Quantity Surveyor
- Awe na uzoefu wa usiopungua miaka mitano (5) katika usimamizi wa majengo.
- Awe anajua kusoma na kutafsiri Michoro na Ramani
- Awe anajua kutumia programme mbalimbali za kusanifu majengo
- Awe ameshasimamia ujenzi wa majengo ya ghorofa.

b) Kazi zakufanya:


- Kusimamia shughuli zote za ujenzi kwenye eneo la ujenzi wa jengo la Ofisi za Halmashauri pamoja na kutoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi kwa Mkurugenzi.

Masharti Mengine.

- Msimamizi wa kazi anatakiwa kuwepo site kuangalia kazi muda wote wakati fundi anaendelea na kazi na kutoa maelekezo pale atakavyoona fundi anaenda isivyo.
- Anatakiwa kulipwa kwa kipindi ambacho kazi za ujenzi zinafanyika na endapo kazi zitasimama nae malipo hayataendelea.
- Barua zitakazoletwa kwa mkono hazitapokelewa.
- Msimamizi wa kazi atatakiwa kutaja kiwango cha malipo anachohitaji kulipwa kwa siku.
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **25/5/2021** saa **9:30** alasiri.
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anwani ifuatayo yakiambatana na wasifu binafsi (CV) na vyeti vya Taaluma na nakala itumwe kwa Email:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Singida,
S.L.P. 27,
SINGIDA.
E-mail: ded.singidadc@singida.go.tz

Imetolewa na:


Rashid M. Mandoa
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
SINGIDA

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
SINGIDA

NB: Tangazo hili linapatikana kwenye **mbao zote za matangazo** za Halmashauri ya Wilaya ya Singida na kwenye tovuti (website) ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida ambayo ni **www.singidadc.go.tz**